Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii & Mfumo wa Mchakato

Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejeshaji katika Mandhari ya Misitu ya Tanzania

Muhtasari wa Utendaji

Utangulizi

Mradi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejeshaji katika Mandhari ya Misitu ya Tanzania (FOLUR) unafanyika kote Zanzibar na Tanzania Bara ukilenga mandhari mbili zilizopewa kipaumbele, na ukiunganisha na hatua za kitaifa za kushughulikia masuala ya kibiashara na mnyororo wa thamani ili kupunguza uharibifu na ukataji misitu katika mandhari hizi, na kwa ujumla kusaidia maendeleo ya kilimo cha Tanzania.

FOLUR itapewa fedha kwa sehemu na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) na WWF ndiye Wakala Mtekelezaji wa mradi huu uliopendekezwa wa GEF. Kwahiyo, Mfumo wa Kuhifadhi Mazingira na Jamii wa WWF, kama ulivyoelezwa kwa kina katika Sera na Taratibu za Hifadhi Jumuishi (SIPP), unatumika kwenye mradi, na unahitaji maandalizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) pamoja na Mfumo wa Mchakato (PF)

Madhumuni ya ESMF/PF

- *ESMF*: Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii una madhumuni ya kuainisha misingi, taratibu na hatua za kupunguza ili kushughulikia athari za mazingira na jamii zinazohusiana na mradi kwa mujibu wa sheria na kanuni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) pamoja na Mfumo wa Hifadhi ya Mazingira na Jamii wa WWF. Kwakuwa wigo sahihi wa shughuli zitakazotekelezwa kama sehemu ya mradi utaamuliwa wakati wa awamu ya utekelezaji, athari maalum za eneo za kijamii na kimazingira hazina uhakika katika hatua hii. Hivyo, maandalizi ya Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii maalum kwa eneo haitawezekana katika hatua hii., na ESMF ina ulazima wa kuweka taratibu za kushughulikia athari mbaya za jamii na mazingira zinazoweza kujitokeza wakati wa shughuli za mradi. ESMPs maalum kwa ajili ya maeneo zitaendelezwa kwa kufuata mwongozo uliotolewa na ESMF wakati wa utekelezaji wa mradi.
- *PF:* Mradi unachochea Viwango vya WWF kwenye Vizuizi vya Kufikika na Makazi Mapya kama utaweza kuzuia au kuathiri ufikiaji wa mali asili na shughuli za kutafuta maisha za Watu Walioathirika na Mradi (PAP). Mfumo wa Mchakato (PF) huu unaelezea mchakato ambao jamii itayoathirika itashiriki kwenye utambuzi, ubunifu, utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli za mradi zinazohusika na hatua za kupunguza. Kusudi la PF ni kuhakikisha ushiriki wa Watu Walioathirika na Mradi (PAP) wakati inatambua na kulinda maslahi yao na kuhakikisha kuwa hayazidi kuwa mabaya zaidi kutokana na mradi.

Methodolojia

ESMF/PF iliandaliwa kwa kuzingatia: a) Mapitio ya sera za WWF SIPP na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za Tathmini ya Mazingira na Jamii; na b) mashauriano na majadiliano ya vikundi yalifanyika Septemba na Oktoba 2020 na wadau 136 katika ngazi ya Wilaya na Vijiji/Shehia.

ESMF/PF inatumia matokeo ya mashauriano, na kwenye sheria na kanuni husika za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na SIPP. *Ili kuepuka kurudia na kwa urahisi wa kumbukumbu, vipengele vya ESMF na PF vimeunganishwa katika nyaraka moja.*

Maelezo ya Mradi

Madhumuni ya mradi ni kuhamasisha mbinu jumuishi ambayo inaunganisha vipengele vya mifumo ya chakula endelevu na minyororo ya usambazaji isiyo ya ukataji miti, na upangaji mpana zaidi katika ngazi ya mandhari, usimamizi na urejeshaji, kwa ajili ya kuhifadhi huduma za mfumo ikolojia katika baadhi ya maeneo ya Tanzania ambayo ni muhimu kwa kilimo cha mpunga.

Mradi umegawanyika katika vipengele binafsi vinne:

- Kipengele cha 1: Kuendeleza Mifumo Jumuishi ya Usimamizi wa Mandhari (ILM), pamoja na kuendeleza mipango ya matumizi ya ardhi na mipango ya ulinzi wa maji inayohusika, na kuanzisha mazingira wezeshi yatakayotoa motisha kwa ushiriki wa sekta binafsi kuelekea shughuli endelevu za usimamizi wa mandhari.
- Kipengele cha 2: Kukuza mbinu za uzalishaji chakula endelevu na minyororo ya thamani inayohusika, ikilenga kwenye kuendeleza minyororo ya thamani/usambazaji endelevu na inayojumuisha jamii kwa ajili ya sekta ya uzalishaji mpunga.
- Kipengele cha 3: Hifadhi na urejeshaji wa makazi ya asili, pamoja na kuendeleza na kutekeleza shughuli thabiti za urejeshaji mandhari katika mandhari zinazolengwa kwa kupitia mipango ya matumizi bora ya ardhi na maji iliyopewa kipaumbele, na ushirikishaji ulio hai wa jamii na sekta binafsi.
- Kipengele cha 4: Uratibu wa mradi na Ufuatiliaji **&** Tathmini, unalenga kwenye uratibu, ushirikiano, ufuatiliaji na tathmini, pamoja na ushirikishaji wa maarifa, mafunzo, na usanisi na mawasilisho ya uzoefu Kitaifa na Kimkoa. (angalia sehemu inayofuata).

Wasifu wa Eneo la Mradi

Mradi unalenga mandhari mbili zilizopewa kipaumbele: Wilaya ya Kilombero iliyo ndani ya bonde dogo la Kilombero katika Tanzania Bara (Hekta 1,356,130), na Wilaya za Kaskazini A/Kaskazini B zilizopo Zanzibar (Hekta 43,100). Mandhari zote mbili zimelengwa mahsusi kwa kilimo cha mpunga, kama zinavyoungwa mkono na mipango mbalimbali inayoongozwa na serikali na sekta binafsi.

Bonde la Kilombero ni mfumo ikolojia wa ardhi oevu ya asili inayojumuisha idadi kubwa mno ya mito, ambayo inatengeneza uwanda mkubwa wa mafuriko ya maji baridi wa msimu wa nyanda za chini katika Afrika Mashariki. Uwanda wa mafuriko unachukua tambarare ya chini ya Bonde la Kilombero kati ya mita 210 – 250 juu ya usawa wa bahari. Wilaya ya Kilombero (Bara) ina idadi ya watu 407,880. Makabila makuu ni Wapogoro, Wandamba, Wabena, na Wambunga na wengine kadhaa kwa sehemu ndogo. Wafugaji na wafugaji wakulima (Wamasai, Wasukuma na Wabarabaig) pia wapo katika Mkoa wa Morogoro ndani ya Kilombero. Ingawa makundi haya yanaweza kufikiriwa kama makundi ya makabila ambayo ni tofauti, wao sio watu wa asili ambao ni tofauti na wana haki sawa kwenye matumizi ya rasilimali kama makabila mengine yaliyopo. Idadi kubwa ya watu (hasa vijijini) katika Bonde la Kilombero ni wakulima wadogo wadogo wa mahindi na mpunga, pia na uvuvi na mifugo.

Shughuli za mradi kwa Zanzibar zitafanyika Unguja, kisiwa kirefu kilicho chini chenye matuta madogo madogo kando ya mhimili wake wa kati wa kaskazini–kusini. Minazi na uoto mwingine umefunika uso wa ardhi. Kisiwa cha Unguja kimegawanyika katika mikoa mitatu na Wilaya sita (Mjini, Magharibi, Kati, Kaskazini A, Kaskazini B, na Kusini). Shughuli nyingi za mradi zipo Wilaya ya Kaskazini A na Kaskazini B. Makadirio ya idadi ya watu katika Wilaya ya Kaskazini A ilikuwa 105,880 (8% ya idadi ya watu Zanzibar). Wilaya za Kaskazini A na Kaskazini B zina makabila mchanganyiko. Makabila yanayopatikana katika Shehia ya Kilombero ni Washirazi/Waswahili na mchanganyiko wa makabila mengine ya kibantu kama Wanyamwezi, Wasukuma, Wazaramo, Wandengereko; wakati katika Shehia ya Kikobweni kuna Watumbatu na makabila mengine mchanganyiko pamoja na makabila ya kibantu. Kilimo ndiyo kazi iliyo kuu.

Makundi makubwa yaliyo katika mazingira magumu katika maeneo yote mawili yanajumuisha wanawake (wajane, wajawazito), wenye ulemavu, vijana, watoto (pamoja na yatima), kaya maskini, kaya zinazoongozwa na wanawake, wazee, na makabila ya wafugaji/wafugaji wakulima. Chanzo cha kuwa kwenye mazingira magumu ni jinsia, umri, ulemavu, ugonjwa, ukosefu wa kipato na rasilimali, ukosefu wa ajira, na maisha ya kuzururazurura.

Sera, Taratibu na Miongozo ya Mazingira na Jamii

Sheria na Taratibu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) na za WWF SIPP ambazo zitatumika kwenye mradi, lakini kwa kusudi la utekelezaji wa FOLUR, kanuni na taratibu za SIPP zitatumika katika kesi zote zenye mapungufu.

Sera na Sheria za URT zitakazotumika

- *Usimamizi wa Mazingira*. Tanzania: Sera ya Taifa ya Mazingira (1997), Mkakati wa Hifadhi wa Taifa kwa Maendeleo Endelevu, Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira. Zanzibar: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu Na. 2 ya 1996 na Sheria ya Hifadhi na Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Na. 10 ya 1996; Sera ya Misitu ya Zanzibar ya 1995 (imepitiwa 2013); Sera ya Mazingira ya 1992 (imepitiwa 2012); na Sera ya Uvuvi. Mpango Kazi wa Mazingira Zanzibar, Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Zanzibar (2009-2020), Mkataba wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu.
- *Usimamizi Jumuishi wa Mandhari*: Katika Tanzania Bara, usimamizi na matumizi ya ardhi unaongozwa na baadhi ya sheria zikijumuisha Sera ya Kitaifa ya Ardhi (1995), Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 (2007), na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 (1999). Kwa Zanzibar, Tume ya Ardhi ina mamlaka ya kupanga na kusimamia ardhi ndani ya Zanzibar.
- *Upatikanaji wa Ardhi na Makazi*. FOLUR haitafanya upatikanaji wowote wa ardhi au makazi, lakini baadhi ya shughuli zake zinaweza kuathiri riziki na shughuli za kiuchumi za watu watakaoathirika na Mradi (PAP) ambao wanaishi ndani ya maeneo ya mradi. Katika Tanzania Bara, sheria itakayotumika inayohusiana na makazi na fidia ni Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, Sehemu ya 156, wakati Zanzibar ni Sheria ya Umiliki wa Ardhi (1992), Sehemu ya 5(4).
- *Ushiriki wa Jamii*. Sera mbalimbali za Kisekta za Taifa zimesisitiza haja na umuhimu wa kushirikisha wadau hasa kutoka kwenye ngazi ya mtaa (chini) katika shughuli za maendeleo. Hii inajumuisha Sera ya Taifa ya Mazingira (1997), Sera ya Taifa ya Ardhi (1995), Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (2007), Sera ya Kilimo (2013), Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji (2013), Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (2009), Sera ya Misitu Tanzania (1998).
- *Watu wa Asili*. Tanzania haitambui kuwepo kwa watu wa asili, ingawa Tanzania ni makazi ya makabila 125-130 tofauti. Hakuna sera au sheria maalum ya kitaifa kuhusu watu wa asili isipokuwa Wahdzabe, Wabarabaig, Wasandawe na Wamasai ni makundi machache Tanzania. Makabila yote hutendewa sawa katika suala la upatikanaji wa maliasili. Kilombero kuna

wafugaji (mf. Wamasai na Wabarabaig) ambao wanahamahama na mifugo yao kutoka eneo moja hadi lingine.

Viwango vya Hifadhi na Taratibu za WWF zinazohusika

Viwango vya Hifadhi vya WWF vinahitaji kwamba athari zozote mbaya za kimazingira na kijamii zinatambuliwa na kuepukwa au kutatuliwa. Sera za Hifadhi ambazo zinahusika na mradi ni kama ifuatavyo: Kiwango cha Usimamizi wa Vihatarishi vya Mazingira na Jamii; Kiwango cha Ulinzi wa Makazi Asili; Kiwango cha uhamishaji upya bila hiari; Kiwango cha Watu wa Asili; Kiwango cha Afya na Usalama wa Jamii; Kiwango cha Usimamizi wa Visumbufu; Kiwango cha Rasilimali za Kitamaduni; Kiwango cha Mfumo wa Uwajibikaji na Malalamiko; Kiwango cha Ushauri wa Umma na Ufichuzi; na Kiwango cha Ushiriki wa Wadau.

Mapungufu kati ya Sheria na Sera za URT na za WWF SIPP

Kwa ujumla, sheria, sera, na miongozo ya URT ipo sambamba na mahitaji ya hifadhi ya mazingira na jamii ya WWF:

- Kuhusiana na athari za mazingira, hakuna utata kati ya sheria na taratibu za URT na za WWF SIPP, ingawa mahitaji ya WWF SIPP ni mapana zaidi. Kwa mfano, WWF SIPP inahitaji uchambuzi wa kina wa athari za mazingira na kijamii ya shughuli maalum za mradi kwenye mazingira na kwa jamii ya wenyeji kabla shughuli haijapitishwa rasmi na fedha yoyote kutolewa.
- Kuhusiana na athari za kijamii, tofauti ya msingi kati ya sheria na taratibu za URT na za WWF SIPP inatajwa kwenye hadhi ya wasio na hatimiliki na matumizi ya ardhi yasiyo rasmi, na kujitolea katika mchakato wa utoaji maamuzi shirikishi. Kwanza, kulingana na WWF SIPP, watumiaji wote wa ardhi na maliasili (ikijumuisha watu ambao hawana hati rasmi ya ya kisheria ya umiliki au haki ya matumizi) wana ustahiki wa aina fulani ya msaada au fidia iwapo mradi utaathiri vibaya maisha yao. Sheria za URT zinatambua ustahiki wa wamiliki ardhi au watumiaji rasmi kupata fidia katika hali kama hii. Pili, WWF SIPP inahitaji mashauriano ya kina na jamii kama sehemu ya maandalizi ya nyaraka mbalimbali za hifadhi wakati wa shughuli za mradi. Sheria za URT hazijumuishi mahitaji ya namna hii.

Katika hali zozote za mgogoro au tofauti, mahitaji ya WWF ndiyo yatatumika kwa makusudi ya Mradi wa FOLUR, juu ya sheria na taratibu za URT.

Mpangilio wa Utekelezaji

Idara ya Misitu na Nyuki (FBD) ya Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) itakuwa Wakala Mtekelezaji Mkuu wa Mradi kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango, ambaye ni mpokeaji.

Washirika wa utekelezaji wakuu wa mradi wanajumuisha Kitengo Kikuu cha Usimamizi wa Mradi (PMU), kilichopo MNRT/FBD, na Vitengo viwili vya Uratibu wa Mandhari (LCU) vya Kilombero na Unguja.

- Kazi za kila siku za usimamizi na utekelezaji wa mradi itakuwa ni jukumu la Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kilichopo ndani ya ofisi za MNRT.
- Utekelezaji wa mradi katika ngazi ya mandhari utasimamiwa na Vitengo vya Uratibu wa Mandhari (LCUs), ambavyo vipo Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero (Mandhari ya Kilombero) na MANRLF/DFNR (Mandhari ya Unguja).
- Kamati ya Uendeshaji ya Mradi (PSC) ambayo Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu wa MNRT itatoa uangalizi na mwongozo wa kimkakati wa mradi.
- Jukwaa la Wadau Mbalimbali la Kilombero lililopo litafanya kazi kama Kamati ya Ushauri ya Mandhari (LAC), ambayo itasaidia Kilombero LCU kwa upande wa mikakati

ya mradi, mpangokazi na utekelezaji kutoka kwenye mitazamo ya washirika wa mradi, pia watahakikisha kufikiwa kwa upana zaidi majimbo husika ya washirika wa mradi.
- Kama Wakala Mtekelezaji wa GEF, Wakala WWF atatoa usimamizi wa kiufundi na fedha na msaada wa kutekeleza mradi na msaada kwenye masuala yanayoathiri utekelezaji wa mradi kwa ubora na kwa wakati muafaka.

Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (PMU) cha FOLUR kitafanya manunuzi ya huduma za Mtaalamu wa Muda wa Hifadhi ya Mazingira na Jamii (ESS). Mtaalamu huyo (ESS) atawajibika kwa Mkurugenzi wa PMU, na atatoa msaada wa masuala ya hifadhi kwa PMU na LCUs zote mbili.

Hifadhi

Mpangilio maalum na majukumu yanayohusiana na utekelezaji wa mahitaji ya ulinzi wa mazingira na jamii, kama yalivyoelezwa katika ESMF/PF hii ni kama ifuatavyo:

- Wakala Mtekelezaji Mkuu (MNRT/FBD): Ana majukumu ya jumla ya kuhakikisha kuwa hifadhi ya mazingira inatekelezwa.
- Kamati ya Uendeshaji ya Mradi: Ina uangalizi wa ujumla na kufuatilia kulingana na masharti ya hifadhi; kusaidia na mapendekezo maalum kwenye masuala ya hifadhi endapo yatahitajika.
- Wakala WWF GEF: Ana uangalizi wa jumla na kufuatilia kulingana na masharti ya hifadhi; kusaidia na mapendekezo maalum kwenye masuala ya hifadhi endapo yatahitajika.
- PMU: Itahakikisha kuwa hati za zabuni na mikataba zinajumuisha vifungu maalum au masharti yanayohusika ya hifadhi ya mazingira na jamii kama yalivyowekwa wazi kwenye mfumo (ESMF); Kutekeleza na kusimamia ESMF na mipango mingine ya hifadhi; Kutoa ripoti za uhifadhi kwa Wakala Mtekelezaji; Kumsimamia Mtaalamu wa Mazingira na Jamii (ESS), na kusaidia Vitengo vya Uratibu wa Mandhari (LCUs); Kutekeleza Utaratibu wa kushughulikia Malalamiko (GRM); Kuweka wazi nyaraka za uhifadhi; kutoa taarifa za utekelezaji na zinazolingana na uhifadhi kwa PSC na Wakala WWF.
- Mratibu wa LCU: Majukumu ya jumla kulingana na Mfumo wa Hifadhi (ESMF) na nyaraka nyingine zilizoambatishwa kwenye ripoti hii; Kupembua shughuli zote za mradi ili kutambua athari za kimazingira na kijamii; Kuchangia kwenye maandalizi ya nyaraka za uhifadhi (Mipango maalum ya eneo [ESMPs] au Mipango ya Urejeshaji Maisha [LRPs]) kama inavyohitajika; Kuhakikisha ujumuishaji wa mahitaji ya uhifadhi katika hati zote za zabuni na mikataba ya mradi; Kufuatilia wakandarasi kufuata mahitaji ya uhifadhi; Kufanya mikutano ya mashauriano na wadau wenyeji kama inavyohitajika; kuwataarifu, kuwapa taarifa juu ya maendeleo ya shughuli za mradi ya hivi karibuni; kufanya ukaguzi wa maeneo wa mara kwa mara; Kutoa ripoti ya utekelezaji wa masuala ya uhifadhi na kukubaliana na Mtaalamu wa ESS na Mkurugenzi wa PMU; Kuhakikisha utekelezaji wa Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko (GRM) na usambazaji wa taarifa kuhusiana na GRM miongoni mwa jamii wenyeji.
- Mtaalamu wa ESS: Kupitia mpango kazi wa mwaka na kupembua miradi midogo ya jamii/binafsi iliyopangwa pamoja na athari zake za kimazingira/kijamii, ili kutambua vihatarishi vya uhifadhi na kuanzisha shughuli za upembuzi; Kusaidia Waratibu wa LCU katika kutekeleza masharti ya uhifadhi na kuchuja shughuli za mradi; Kuandaa na kuchangia nyaraka za uhifadhi kama inavyohitajika kufuatana na ESMF/PF, na kwa kushirikiana kwa karibu na PMU na Waratibu wa LCU; Kuhakikisha kuwa mashauriano na jamii yanafanyika kwa namna ambayo ni jumuishi na shirikishi, na kumbukumbu zinawekwa vizuri; Kufuatilia hali ya utekelezaji wa masuala ya uhifadhi, na kuhakikisha kuwa miradi midogo inatekelezwa kufuatana na mbinu bora na miongozo iliyowekwa na ESMF/PF; Kuendesha Utaratibu wa Mradi wa Kushughulikia Malalamiko (GRM); Kufanya ziara za lazima za kufuatilia utekelezaji wa shughuli za mradi na zinazokulingana na mahitaji ya uhifadhi; Kutoa msaada wa uwezo kwa PMU, LCU, na kwa wadau wengine wa mradi wanaohusiana na masuala ya kimazingira

na kijamii; Kutoa taarifa ya jumla ya utendaji wa kuhifadhi kwa Kamati ya Uendeshaji wa Mradi, Wakala WWG GEF na wadau wengine kama inavyolazimu.

Athari za Mazingira na Hatua za Kupunguza zinazotarajiwa

Mradi wa FOLUR unataka kuzipa nguvu mbinu za kuhifadhi mazingira katika mandhari mbili zinazohusika, na hivyo unatarajiwa kutoa matokeo makubwa chanya ya mazingira. Athari ndogo hasi na maalum kwa eneo zinaweza kujumuisha yafuatayo:

Shughuli zinazofaa chini ya Matokeo 2.2.2.: Mipango endelevu ya mnyororo wa thamani iliyopewa kipaumbele katika sekta ya uzalishaji mpunga kufadhiliwa na kuendeshwa

Matokeo haya yanajumuisha shughuli mbalimbali zinazostahiki ambazo zinaweza kuleta athari mbaya za mazingira, kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1 hapo chini.

Jedwali 1: Athari mbaya za mazingira chini ya matokeo 2.2.2.

Kundi	Shughuli zinazowezekana	Uwezekano wa athari mbaya za mazingira	Hatua za kupunguza zinazopendekezwa
Pembejeo za Kilimo	• Utambulisho wa aina bora za mbegu za mpunga kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) • Kukuza mifumo rafiki zaidi wa mazingira ya viuatilifu na mbolea	• Aina mpya za mbegu kusababisha uharibifu kwenye udongo na kuharibu mimea ya mahali husika, kupunguza rutuba ya udongo, n.k. • Viuatilifu na mbolea kutumiwa vibaya na kuharibu udongo, kusababisha uharibifu wa mimea ya mahali husika na aina zisizolengwa, kuzalisha taka, na inaweza kuchafua maji kwenye mkondo wa chini	• Tathmini ya usahihi wa mbegu kwa upande wa bioanuwai, ufanisi wa maji, mahitaji ya ndani, kudumu, n.k. • Kuhakikisha kuwa mbegu zinazolingana zinapandwa • Kujenga uwezo wa Watekelezaji Washirika ili kuhakikisha ufahamu kamili na maarifa katika matumizi na athari za viuatilifu na mbolea zilizochaguliwa • Kuhakikisha kuwa hakuna uharibifu wa bahati mbaya unaosababishwa kwa mimea ya mahali au aina zisizolengwa
Mbinu za mashambani	• Kufanya majaribio ya mbinu za uzalishaji mpunga zenye ufanisi wa maji, kuboresha usawa wa shamba, uboreshaji/ujenzi na uendeshaji wa miundombinu sahihi ya kuingiza na kutoa maji shambani • Kufanya majaribio ya kuimarisha mbinu za kudhibiti rutuba ya udongo • Kukuza uvunaji maji na umwagiliaji wenye ufanisi kwa kupitia msaada wa kiufundi na kutoa ruzuku ya miundombinu midogo	• Athari zinazohusiana na ujenzi (mf. Uchafuzi, vumbi, kelele, taka, n.k.) zinazotokana na uchimbaji wa ardhi, taka na udhibiti wa vifaa katika eneo. • Uharibifu wa udongo na/au uharibifu kwa mimea ya mahali husika • Taka ngumu kama pumba za mpunga	• Hatua za utaratibu ili kupunguza usumbufu wa kelele, kudhibiti ukusanyaji taka, kuzuia uchafuzi wa vumbi na uchafuzi wa maji • Hatua za kuzuia mmomonyoko wa udongo, maporomoko ya ardhi, na mafuriko
Shughuli baada ya mavuno	• Kufadhili ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia baada ya mavuno. • Kutumia tena taka za pumba za mpunga kutengeneza matofali yanayofaa ambayo ni rafiki kwa mazingira, vifaa vya ujenzi au chakula cha mifugo	• Athari zinazohusiana na ujenzi (mf. uchafuzi, vumbi, kelele, taka, n.k.) zinazotokana na uchimbaji wa ardhi, udhibiti wa taka na vifaa katika eneo. • Uharibifu wa udongo na/au uharibifu wa mimea ya mahali husika	• Tazama hapo juu

Shughuli zinazofaa chini ya Matokeo 3.1.1: Urejeshaji wa ardhi iliyoharibiwa katika maeneo yaliyopewa kipaumbele kwenye mipango ya mandhari

Athari mbaya za kimazingira katika shughuli hii ni kwamba teknolojia za urejeshaji zinaweza kuathiri vibaya vyanzo vya maji, mifugo na mimea. Athari hizi zinajumuisha kupanda aina vamizi za mimea katika kuboresha ardhi iliyoharibiwa, usumbufu wa makazi ya asili, matumizi yasiyo sahihi ya kemikali za kilimo ya wakulima kutokana na elimu ndogo ya matumizi na utunzaji salama wa viuatilifu, ukataji wa miti na mimea unaweza kuleta athari hasi kwenye mfumo wa ikolojia (mf. maeneo ya malisho yanaweza kupungua)

Hatua za kupunguza athari hizi zinajumuisha: Tathmini ya kufaa kwa spishi (aina za mimea) kwa upande wa bioanuwai, ufanisi wa maji, moto wa misitu, mahitaji ya ndani, unyeti wa kiutamaduni, kuishi, n.k.; kuhakikisha spishi za asili tu zinapandwa; kutekeleza hatua za kuzuia uchimbaji udongo na usumbufu wa kelele ili kupunguza athari kwenye makazi ya asili; kufanya shughuli za kujenga uwezo na mafunzo ili kuhakikisha matumizi sahihi ya viuatilifu; kuhakikisha kuwa hakuna uharibifu wa bahati mbaya unasababishwa kwenye mimea ya mahali; kutambua maeneo mbadala ya malisho, n.k.

Athari za Kijamii zinazotarajiwa na Hatua za Kupunguza

Mradi huu unategemea kutoa matokeo chanya kwa jamii kwa kuboresha maisha ya vijijini, kuimarisha ustahimilivu wa jamii wa mabadiliko ya tabianchi, kuwezesha jamii kwenye utawala bora wa maliasili. Athari mbaya za kijamii zinategemewa kuwa ndogo na katika sehemu maalum na zinaweza kutokea kama sehemu ya shughuli za Matokeo 1.1.3., 2.2.2. na 3.1. Hizi zinaweza kujumuisha yafuatayo:

1. Migogoro ya Kijamii inaweza kutokea kuhusu vigezo vya kuchagua vijiji vitakavyolengwa (katika Kilombero) na Kuendeleza ya mipango ya msingi ya udhibiti (katika maeneo yote mawili). Hatua za kupunguza zitajumuisha yafuatayo:

- Shughuli za mradi zinaweza kuanzisha migogoro na mivutano kati ya jamii na kati ya wakulima na wafugaji inabidi ifanyike tu baada ya kushauriana na watu wote watakaoathirika.
- Mipango ya Udhibiti ya Jamii inatakiwa kuendelezwa katika namna shirikishi, jumuishi na ya mashauriano ili kuhakikisha haki za ufikiaji zinakubaliwa miongoni mwa wanajamii.
- Mabadiliko yoyote au uwekaji upya wa mipaka unatakiwa ufanyike kwa kuzingatia mashauriano huru na ya awali kwa jamii zitakazoathirika pamoja na mamlaka husika, ambayo yanatakiwa yapatikane kabla ya kumalizika kwa mabadiliko yoyote ya mipaka.
- Kama uwekaji mipaka ardhi utaleta athari hasi kwenye vyanzo vya mapato vya kiuchumi au aina nyingine za maisha ya jamii zitakazoathirika, fidia kamili na kwa wakati inatakiwa kutolewa kwa watu wote binafsi watakaoathirika, bila kujali umiliki wao rasmi wa ardhi, kulingana na Mpango wa Urejeshaji Maisha (angalia hapo chini). Fidia inatakiwa kupigiwa mahesabu kwa kuzingatia thamani mbadala ya maisha hayo (thamani ya soko pamoja na gharama zozote za ubadilishaji)
- Shughuli za kukuza ufahamu na shughuli za kujenga uwezo zinatakiwa kutekelezwa kuhusu haki na kanuni za usimamizi wa ardhi na malisho

2. Baadhi ya Mipango ya Usimamizi inaweza kujumuisha *upatikanaji wa vikwazo vya maisha* (upatikanaji wa na matumizi ya maeneo ya malisho, pia upatikanaji wa na matumizi ya vyanzo vya maji ya umwagiliaji). Hatua za kupunguza zaitajumuisha yafuatayo:

- Msaada unaohusiana na riziki wakati wa utekelezaji wa mradi utatolewa kwa kaya (HH) za jamii zote na wafugaji/wafugaji wanaolima walioathirika na vikwazo vinavyotokana na mradi vya kufikia maliasili na ya jamii katika maeneo yaliyolengwa. Waratibu wa LCU pamoja na masuala ya kiufundi kutoka kwa Mtaalamu wa Hifadhi wa PMU watafanya upembuzi wa shughuli zote zilizopangwa kufanyika kama kuna uwezekano wa vikwazo vya kufikia kwa jamii wenyeji. Kama upembuzi utathibitisha na kutambua kaya zilizoathirika kutokana na vikwazo vya kufikia maliasili, mchakato wa tathmini ya kijamii (SA) kwa kuzingatia mashauriano shirikishi na watu walioathirika utafanyika.
- Kwa kuzingatia matokeo ya upembuzi na tathmini ya jamii, Mpango Kazi ambao kwa kawaida unajulikana kama Mpango wa Urejeshaji Maisha (LRP) utaandaliwa baada ya kufanya mashauriano yenye maana kwa watu walioathirika pamoja na wadau ambayo yatatoa msaada wa kujikimu kimaisha na kugawana faida kwa watu, vikundi na jamii iliyoathirika.

3. Afya na Usalama Kazini na kwa Jamii (kwa mfano, ubora na usambazaji wa maji kwa jamii wenyeji unaweza kushuka daraja, vihatarishi vya usalama vinaweza kuibuka kutokana na shughuli za ujenzi na kutokana na uwezekano wa matumizi ya vifaa hatari. Kupunguza athari hizi, Waratibu wa LCU pamoja na Wakandarasi watekelezaji wanatakiwa kutoa mazingira ya kazi salama na yenye afya, kwa kuzingatia hatari za kimwili, kemikali na kibaolojia ambazo zinatokana na shughuli za mradi, na zenye tishio maalum kwa wanawake.

Utaratibu wa Utambuzi na Usimamizi wa Athari za Mazingira na Jamii

Shughuli zifuatazo hazitafadhiliwa na Mradi wa FOLUR: (i) Shughuli ambazo zitahusisha manunuzi na matumizi ya viuatilifu vilivyo katika makundi IA, IB, au II ya Shirika la Afya Duniani (WHO); (ii) Shughuli ambazo zitahitaji upatikanaji wa ardhi binafsi; (iii) Shughuli zinazohitaji kuhamisha watu kutoka kwenye nyumba zao au biashara zao halali, bila kujali umiliki; (iv) Shughuli ambazo zitahusisha ukataji miti katika kanda za msingi na maeneo muhimu ya maji; (v) Shughuli ambazo zitahusisha uchimbaji mawe na uchimbaji madini; (vi) Shughuli ambazo zitahusisha ukataji miti kibiashara.

Kabla ya kuanzishwa shughuli yoyote ya mradi, Waratibu wa LCU watapaswa kujaza taarifa za kina kuhusu asili ya shughuli na eneo lake maalum katika Fomu ya Ustahiki wa Hifadhi na Upembuzi wa Athari (*Safeguards Eligibility and Impacts Screening Form)*

Kama mchakato wa upembuzi unaonesha kuwa tathmini ya ziada au nyaraka za hifadhi zitatakiwa kuandaliwa, hizi zitatakiwa kufanyika na washirika watekelezaji kabla ya kuanza shughuli. Kama upembuzi umeonesha athari mbaya za kimazingira na kijamii ambazo zinaweza kutokea kutokana na shughuli iliyopangwa, ESMP (Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii) utatakiwa kuandaliwa. ESMP inatakiwa iandaliwe na Mtaalamu wa ESS, akishirikiana na Mratibu wa LCU.

Miongozo ya Kuandaa ESMP

ESMP inatakiwa iandaliwe kabla ya kuanza shughuli za mradi na ufuate kwa karibu mwongozo uliotolewa na ESMF hii. ESMP inatakiwa kuelezea athari za mazingira na jamii zinazotarajiwa kutokeakutokana na shughuli maalum ya mradi, kueleza hatua madhubuti ambazo zinatakiwa kuchukuliwa kuzuia au kupunguza athari hizi, na kubainisha mpangilio wa utekelezaji kwa ajili ya kusimamia hatua hizi (ikijumuisha miundo ya taasisi, majukumu, mawasiliano, mashauriano, na utaratibu wa kutoa taarifa).

Ufuatiliaji

Ulinganifu wa shughuli za FOLUR na ESMF utafuatiliwa kwa kina na vyombo mbalimbali katika hatua tofauti za maandalizi na utekelezaji.

- *Ufuatiliaji katika ngazi ya mradi*. Majukumu ya ujumla ya kutekeleza ESMF na ya kufuatilia kama yanalingana na shughuli za mradi za hifadhi ya mazingira zipo kwa PMU. Mtaalamu wa ESS aliyefanyiwa manunuzi na OMU atasimamia utekelezaji wa shughuli zote za shamba na kuhakikisha kuwa zinafuatana na ESMF.
- *Ufuatiliaji katika ngazi ya shamba*. Waratibu wote wa LCUs watafuatilia kwa kina shughuli zote za shamba, na kuhakikisha kuwa zinalingana kikamilifu na ESMF pamoja na vigezo na masharti kujumuishwa katika vibali vya mazingira vinavyotolewa na Mamlaka za Kitaifa za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT). LCU pia watawajibika kwa wakandarasi wote wa nje na watoa huduma kama sehemu ya mradi kufuata mahitaji ya hifadhi yaliyoainishwa kwenye ESMF/PF na ESMP (kama itakavyotumika)
- *Ufuatiliaji katika ngazi ya utekelezaji wa GEF na ngazi ya utekelezaji wa Wakala.* WWF kama Wakala Mtekelezaji wa Mradi, na MNRT kama Wakala wa Utekelezaji na Mwenyekiti wa Kamati ya Uendeshaji wa Mradi (PSC), wanawajibika kusimamia kufuatwa kwa ESMF.

Ushiriki wa Jamii wakati wa utekelezaji wa Mradi

Hatua za jumla za ushirikishaji wa wadau zimeainishwa kwenye Mpango wa Ushiriki wa Wadau (SEP) wa Mradi

Kwa kuongezea na hatua za SEP, jamii zilizoathiriwa na mradi zinatakiwa zishirikishwe kabla ya utekelezaji wa kila shughuli ambayo itaathiri maslahi, haki, na maisha yao. Shughuli hizo zinatakiwa zitambuliwe na Waratibu wa LCU pamoja na Mtaalamu wa Hifadhi kwa kupitia mchakato wa upembuzi wa hifadhi ya mazingira na jamii. Kama upembuzi utaweka wazi athari mbaya zozote za mazingira na jamii ambazo zinatokana na shughuli iliyopangwa, mashauriano ya jamii yanatakiwa kupangwa yafanyike kabla ya utekelezaji wa shughuli hiyo, ili kuweza kupunguza athari. Shughuli ambazo zitaleta kizuizi au upotevu au riziki zinapaswa kuchochea undelezaji wa Mipango ya Urejeshaji Maisha ya eneo maalum.

Wanajamii watakaoshirikishwa kwenye mashauriano ni wale watu ambao, kama matokeo ya moja kwa moja ya shughuli au mradi mdogo, bila ridhaa yao au uwezo wa kuchagua aidha: (a) watapoteza mali zao au ufikiaji wa mali au ufikiaji wa jamii na maliasili, au (b) watapoteza chanzo cha mapato au njia za kuendeshea maisha iwe wanahama au la kimwili kwenda mahali pengine.

Makundi yaliyo katika mazingira maalum na yaliyotengwa yanapaswa kushirikishwa kikamilifu kwenye mashauriano yanayohusiana na mradi na katika kuendeleza Mipango ya Urejeshaji Mandhari (LRPs). Makundi haya yanajumuisha: Wanawake (hasa wajane na kaya zinazoongozwa na wanawake), vijana, watu wenye ulemavu, wazee (hasa kaya zinazoongozwa na mtu mmoja), na makundi yanayohamahama (Wamasai na Wabarabaig katika Mandhari ya Kilombero), ambao wanaweza wasiwepo kwenye jamii kwa wakati wote.

Kwa mchakato wa ushirikishaji wa jamii kuwa jumuishi iwezekanavyo, ni muhimu kutumia njia mbalimbali inavyowezekana kujulisha wadau wote kupitia matangazo, redio ya kitaifa na televisheni n.k. Mapendekezo maalum na miongozo ya njia za ushirikishaji yametolewa kwenye ESMF.

Utatuzi wa Malalamiko

GRM ya FOLUR itasimamiwa na PMU kwa uratibu na LCUs. Mtaalamu wa ESS atakuwa Msimamizi wa uendeshaji wa GRM katika PCU, na kila LCU itamteua mtu ambaye atawajibika kukusanya na kushughulikia malalamiko ambayo yanashughulikia shughuli katika kila eneo ya mandhari inayoshiriki. Mwongozo wa kuendesha GRM umeainishwa katika ESMF.

Kuarifiwa

Jamii zote zilizoathirika na mradi na wadau wanaohusika watafahamishwa kuhusu mahitaji ya ESMF na masharti sambamba na mahitaji yaliyoainishwa kwenye ESMF

Wakati wa utekelezaji wa FOLUR, Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP) ya shughuli maalum itaandaliwa kwa mashauriano na jamii itakayoathiriwa na mradi na kuarifiwa kwa wadau wote kabla ya wazo la mradi kukamilika.

Bajeti

Gharama za kutekeleza ESMF, ikijumuisha na gharama zinazohusiana na fidia kwa watu walioathiriwa na mradi, zote zitashughulikiwa kikamilifu kutoka kwenye bajeti ya FOLUR. Itakuwa ni jukumu la PSC na PMU kuhakikisha kuna bajeti ya kutosha kwa shughuli zote maalum za kupunguza athari ambazo zitatakiwa kulingana na ESMF.